**FOMU PLUPA L-2** **(r.10)**

**JAMHURI YA KENYA**
**SHERIA YA MPANGO WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI**
**(*Nambari* 13 *ya* 2019)**

## ILALNI KUHUSU KUKAMILISHWA KWA MPANGO WA USTAWISHAJI

Kichwa cha Mpango wa Ustawishaji:

**Kurasimishwa kwa Eneo la utekelezaji wa:**

a) **Mpango wa Nyumba za Gharama Nafuu, Kapsuswa, Awamu ya Kwanza**
b) **Mpango wa Nyumba za Gharama Nafuu Kapsuswa, Awamu ya Pili Nambari ya PDP NRB/17/2025/02**

**ILANI** inatolewa kwamba, kwa mujibu wa hitaji la Sehemu za 13(g), na 69(1) ya Sheria ya Mpango wa Miji na Mpango wa Matumizi ya Ardhi, 2019 ikisomwa pamoja na Notisi ya Sheria Nambari 27 ya 2020, utayarishaji wa mpango uliotajwa hapo juu ulikamilika mnamo Februari 17, 2025.

Mpango huo wa Ustawishaji unahusu eneo lililoko ndani ya Manisipaa ya Eldoret—Kaunti ya Uasin Gishu.

Nakala za Mpango huo wa Ustawishaji ulivyotayarishwa umehifadhiwa kwa ukaguzi na umma, bila malipo, katika Afisi za **Kamishna wa Kaunti ya Uasin Gishu** , **WAZIRI WA KAUNTI Anayesimamia Idara ya Mpango wa Miji na Matumizi ya Ardhi-Kaunti ya Uasin Gishu** na **Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji-Orofa ya 5 Jumba la Ardhi House, Nairobi; kati ya saa mbili za asubuhi (8.00 am) na saa kumi na moja jioni (5.pm), Jumatatu hadi Ijumaa.**

Mtu yeyote ambaye angetaka kutoa maoni au pingamizi kuhusu Mpango wa Ustawishaji uliotajwa hapo juu anaweza kuziwasilisha, kwa maandishi, ili zipokelewe na Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji, barabara ya 1st Ngong' Avenue, Jumba la Ardhi House, S.L.P. 45025-00100, Nairobi au zitumwe kwa njia ya barua pepe: ndpp@ardhi.go.ke ndani ya siku sitini (60) baada ya kuchapishwa kwa ilani hii. Na maoni au pingamizi hizo sharti ziandamanishwe na sababu zilizochangia kutolewa kwazo.

**TAREHE** Februari 25, 2025.

Dkt Peris Mang'ira, PhD, HSC

**MKURUGENZI WA KITAIFA WA IDARA YA MPANGO WA MIJI**